Nipashe Jumanne Agosti 19, 2025 Pg 8

# 'Bodaboda wawe mabalozi wa amani na usalama barabarani'

**Na Issa Mwadangala,** MOMBA

KATIKA jitihada za kuhakikisha usalama wa watumiaji barabara na kulinda taswira ya vijana nchini, madereva wa bodaboda wametakiwa kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia sheria na taratibu za usalama barabarani, huku wakihimizwa kuwa mstari wa mbele katika kulinda amani na mshikamano wa kitaifa.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkaguzi wa Polisi wa Kata ya Mwakakati, Robert Kasunga wakati wa kikao maalumu cha kutoa elimu kwa vijana wanaojishughulisha na usafirishaji abiria kwa pikipiki, maarufu bodaboda.

Mkaguzi Kasunga aliwaasa madereva wa kijiwe cha Zwagwila, kata ya Mwakakati, wilayani Momba mkoani Songwe kuepuka tabia hatarishi ikiwamo kuegesha pikipiki pembezoni mwa barabara kuu ya Tunduma-Sumbawanga, jambo ambalo si tu linahatarisha usalama wao na abiria, bali pia husababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wengine wa barabara hiyo.

"Sheria za usalama barabarani zipo kwa ajili ya kuwalinda ninyi na abiria mnaowahudumia. Hakikisheni mnaendesha kwa tahadhari, mnavaa kofia ngumu (helmet), mnaepuka mwendokasi na mnatambua alama zote za barabarani," alielekeza Mkaguzi Kasunga kwa msisitizo.

Mbali na usalama barabarani, Mkaguzi huyo alizungumzia umuhimu wa vijana hao kujiepusha na aina yoyote ya vitendo vya uhalifu vikiwamo:

Usafirishaji wa bidhaa za magendo, ukabaji au uporaji abiria, Kushiriki shughuli haramu kipindi cha uchaguzi na kusaidia vurugu zinazochochea uvunjifu wa amani.



Bodaboda

"Taswira ya kazi yenu kama bodaboda ni muhimu. Msikubali kutumiwa vibaya, hasa wakati huu tunapoelekea kipindi cha uchaguzi. Ninyi mna nafasi kubwa katika kuhakikisha jamii inabaki salama na yenye utulivu," alionya Mkaguzi Kasunga.

Katika kuimarisha juhudi za maendeleo na kudumisha mshikamano wa kijamii, vijana hao walihimizwa kushirikiana kwa karibu na viongozi wa serikali za mitaa, wazee wa mtaa na vijiji pamoja na wananchi wote katika kuwafichua wahalifu na kuzuia uhalifu kabla haujatokea.

"Elimu yenu na uzoefu mnavyoupata katika kazi ya kila siku, unawapa nafasi ya kufahamu kwa haraka mabadiliko yanapotokea mtaani. Mtoe taarifa mapema pale mnapohisi kuna viashiria vya uhalifu. Hilo ni jukumu la kizalendo," alisisitiza.

Kasunga alihitimisha hotuba yake kwa kuwasihi madereva wa bodaboda kuwa mfano wa kuigwa katika jamii, kwa kudumisha nidhamu, kujiheshimu na kuwaheshimu abiria, kutoa huduma kwa weledi, kuepuka lugha chafu na mizozo isiyo na tija.


"Ninyi ni mabalozi wa usalama, maendeleo na amani katika maeneo yenu. Kazi yenu ni muhimu kwa uchumi wa nchi. Endeleeni kushirikiana, mwendeleze mshikamano, na kuonesha uzalendo katika kila mnachofanya," alisema.

Pg1 Uhuru Jumanne Agasti 19, 2025



**WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, akisafiri kwa treni ya umeme ya kiwango cha Kimataifa (SGR) kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, jana.** (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

Pg 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwasili kwa treni ya Reli ya Kisasa (SGR) katika Stesheni ya Magufuli, Dar es Salaam jana akitokea jijini Dodoma. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

The Guardian August 19, 2025 Pg 8






**sidents of Isela Village in Shinyanga Region look at a bus christened Dreamliner after it was involved in an ident yesterday.** Photo: Guardian Correspondent



Magari na bodaboda yakipita katika daraja la muda katika barabara ya mchepuko kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara ya mwendo wa haraka (BRT) katika Mto Msimbazi, Kigogo, Dar es Salaam jana. (Picha na Venance Nestory).